**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA .**

**FASIHI 102/3**

**TATHMINI YA BUURI MASHARIKI**

**MWAKA 2018**

# MWONGOZO WA KUSAHISHA KARATASI YA TATU.

1. Swali la Lazima

(a) Ulimwengu
Ulimwengu ni kiwanja
Changamoto ulimwenguni. 1x1=1

(b) Istiara/ jazanda- ulimwengu ni kiwanja
Msemo – kutwa kuchwa
Ukinzani/ tanakuzi –wenye raha na tabu.
Uhuishaji – Kichwa kudanganya shingo.
(Zozote 2x1=2)

(c) Inkisari – naratibu – ninaratibu
Ndu zangu – ndugu zangu.
Kuboronga lugha – wenye kitu hatuna – wengine hatuna kitu
Utohozi – shehe – sheikh
- Padre – padre
(2x1=2)

(d) Babu alimshauri kuwa ulimwengu ni uwanja wa balaa uliojaa mambo ya faraja na kusibu. Pia alisema kuwa kuna machache ya kufaidi na mengi ya kuudhi. Kwa hivyo ulimwengu ni kiwanja kwa walio na raha na walio na taabu.
(4x1=4)

(e)
(i) Tarbia – mishororo minne kwa kila ubeti.
(ii) Mathnawi – vipande viwili kwa kila mshororo.
(iii) Pindu – sehemu ya mwisho kuanzia ubeti unaofuata.
(iv) Ukara – Vina vya mwisha vinatiririka na vya kati havitiririki.
(2x1=2)

(f)
(i) Mishororo minne kwa kila ubeti.
(ii) Vipande viwili kwa kila mshororo – ukwapi na utao.
(iii) Lina beti tisa.
(iv) Vina vya mwisho vinatiririka na vya kati vinabadilika.
(v) Lina kibwagizo – cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.
(vi) Mizani ni 8,8 kwa kila mshororo.
(4x1=4)

(g) Masikitiko (1x1=1)

(h) Kufahamisha watu hali ilivyo ulimwenguni- kwamba kuna mazuri na mabaya ili wajihadhari.
(1x2 = 2)

(i) Malofa – maskini
(ii) Ndubu – upumbavu.
(2x1=2)

2. ***TAMTHILIA.***

***KIGOGO-***

(i)
- Maneno ya Majoka
- majoka alikuwqa amezirai. Anazungumza na nyanyaka na anatibiwa na dakatari.
- Alikuwa akipelekwa hospitalini.
- Alizirai alipofahamishwa kuhusu kifo cha mwanaye Ngao Junior.
- Majoka anahisi kuwa babu yake hamfahamu mke wake.

(ii)
- Majoka anahisi mkewe Husda hampendi bali anapenda mali zake.
- Majoka hampendi Husda bali alilazimishwa kumuoa.
- Majoka anapenda Ashua.
- Majoka alisabisha kifo cha Jabali ikasingiziwa ni ajali ya barabarani.
  - Kenga ana unafiki anapomhudumia majoka kwani mambo yanapoharibika anamtoroka.
  - Mama pima alifahamu anawapunja walevi akifahamu madhara ya pombe haramu.
  - Sudi alikusudia kutengeneza kinyago ndio akakataa pendekezo la Majoka la kutengeneza kinyago cha Marara.
  - Chopi alipewa kazi ya kummaliza Tunu jambo tunalofahamu baada ya kitendo chake kutofaulu.
  - Majoka na watu wake wanaendelea kununulia walevi pombe ili waendelee kumuunga mkono.
  - Shuleni mwa majoka wasomi hawafunzwi kwani wanatumia dawa za kulevya na kuwa wajinga.
  - Twafahamishwa soko lilifungwa kwa sababu ya uchafu lakini lengo lilikuwa kulinyakua ili kujenga hoteli ya kifahari.
  - Ashua alimtembelea Majoka kukiwa na njama ya kumzuia ili waweze kumlazimisha sudi kutengeneza kinyago cha marara.
  - Boza alikuwa ametumwa kwa wachongaji wa vinyago lakini hakuwafahamisha – ukweli unafahamika Kenga anapowatembelea.

(7x2=14)

3. (i) Askari – wanawanyonga waandamaji.
(ii) Vyombo vya habari – vimefungwa na kuwachwa cha mzalendo.
(iii) Kutumia washauri – kenga.
(iv) Vitisho – sudi, tunu
(v) Mauaji – Jabali.
(iv) Kupumbaza kwa kutumia vileo pombe,
(vii) Vishawishi – hongo kwa wanaomuunga mkono Kenga anaahidiwa kipande sokoni.
(viii) Uvumi – vikaratasi vya kuonya watu wahame.
(ix) Jela – Kufungia /kuzuiliwa washukiwa.
(x) Tenga tawala – kutumia Boza, ngurumo, mama pima.
(xi) Kutumia watu wa familia na marafiki – katika kutawala- Kenga, mama pima.
(xii) Udikteta – kulazimishwa watu – kutosikiliza raia . hakusikiza maneno ya Tunu.
(xiii) Kubana raia kiuchumi – kufunga soko, kodi ya juu,
(xii) Kutoa ahadi ambazo hazitimizwi.
(10x2= 20)

***<u>Riwaya .</u>***

4. ***Kidagaa.***

a) (i) Maneno haya yalisemwa na Dora.
(ii) Alikuwa akimwambia mumewe mwalimu majisifu.
(iii) Wakiwa nyumbani.
(iv) Imani alikuwa ameondoka na dora alikuwa na Kazi nyingi.

b) Msemaji ni majisifu.
(i) Mlevi
(ii) Mzembe
(iii) Msomi
(iv) Mwenye kiburi.
(v) Mwenye hasira – alimhifadhi Amani.
(vi) Muasi dini.
(vii) Mpyoro – kutusi watoto wake.
(viii) Mdanganyifu
(ix) Ni mwizi.

c) (i) Ni walezi – Dora
(ii) Wavumilivu - Dora na Bi. Zahura wavumilia waume zao.
(i) Washerati - lowela
(ii) Washauri – Bi. Zuhura anamshauri mumewe.
(iii) Wenye bidii – Dora alijitahidi kulea wanawe
(vii) Wenye huruma –Imani anasaidia Amani kwa kukilea kitoto
(viii) wenye mapuuza – wauguzi walikataa kutibu kitoto uhuru.
(Viiii) Ni wanamapinduzi kama imani.
(iv) Ni wakarimu – Bi. Zihura alituma maziwa na nguo kwa kitoto uhuru.
(v) Wenye msimamo dhabiti – imani alikataa kuhudhuria sherehe.
(6x2=12)

5. (a) ***SADIFA***.

(i) Amani na imani kukutana katika ziwa mawewa.
(ii) Walipokutana kila mtu ana shida . amani alitaka kujiua na amani alikuwa akienda kutafuta mwizi wa mswada wake.
(iii) Kaptula ya Dj kuliwa na ng'ombe na Amani akawa na shati la kumsaidia.
(iv) Dj ambaye alisaidiwa na shati kufahamu alikotaka kwenda Amani (mtemi Nasa Bora)
(v) Dj, Amani na Imani wanampata Mtemi Nasaba Bora akiwa anataka kuondoka.
(vi) Wanapomkuta wanamsaidia kusukuma gari lake lililokuwa limekataa kunguruma.
(vii) Amani kupata kuwa mtemi Nasaba Bora anahitaji mtu wa kuchunga kazi (kuna nafasi ya kazi)
(viii) Amani Kupata kuwa mtemi Nasaba Bora inahitaji mtu wa kuchunga kazi (kuna nafasi ya kazi)
(ix) Imani kukuta kwake mwalimu majisifu kunahitaji mfanyikazi – anapata kazi.
(x) Amani na Imani wameajiriwa na ndugu.
(xi) Amani kukuta Gaddafi akitaka kumwangamiza Mtemi Nasaba bora na kumsaidia Mtemi – Gaddafi alimjua Amani.
(xii) Sadfa Dj. Kupita kwa Amani na akapata kumtuma kumwita Imani.
(xiii) Sadfa Amani na Amu yake Yusufu kukutana katika jela moja ambayo Yusufu alimwelezea Amani zilipokuwa hatihiliki katika kasri la nasaba Bora.
(xiv) Mtemi anawasili wakati Amani akiwa chumbani na mkewe akafikiria ni wapenzi.
(xv) Amani kusahau barua ya Amani mezani, majisifu akaipata na kujua siri ya mswada imegundulika.
(xvi) Majisifu kumpa Amani kitabu "kidagaa kimememwoza asome alipomwomba asome kilitokana na mswada wake.
(xvii) Imani kusikia matangazo ya mpira akiwa katika ser na akaweza kusikia habari za kakake cesechwe makweche.
(xviii) Mwalimu majisifu kwenda nyumbani na gazeti lililokuwa na habari kumhusu chwechwe makweche nduguye Imani na Imani kulisoma.

(xix) Siku ambayo imani anaandamana na majisifu kwenda hospitalini, ndiyo Amani alipewa ruhusa kurudi nyumbani naye akampa makao. (10x1=10)

b) Mbinu Rejeshi.

(i) Imani kumweleza Amani namna nyumba yao ilivyochomwa.
(ii) Tunadokezwa jinsi fao alivyoibiwa mtihani.
(iii) Baada ya imani kunywa maji ya mto kiberenge kunadokezwa asili ya mwiko kutokunywa maji.
(iv) Maelezo kuhusu namna Majununi alivyojengea mpezi wake michele kasri.
(v) Maelezo jinsi mwalimu majisifu pamoja na nduguye alilelewa na babake kasisi.
(vi) Tumerejeshwa katika maisha ya Fao kuhusu kudunga msichana mimba, kwenda kusomea ng'ambo.

(vii) Tumerejeshwa kwa mwalimu Majisifu jinsi alifanya kazi kwa mashirika kadhaa kabla ya kuwa mwalimu.
(viii) Tumerejeshwa nasaba bora alivyomburura paka alipokula nyama yake alipokuwa akisherekea gari lake jipya.
(ix) Kisa cha jinsi Nasaba Bora alivyopata kazi kuwa na uhusiano mwema na mudir kiongozi wa wakati huo.
(x) Tunaelezwa jinsi matuko weye alivyopigana vita humo Burma.
(xi) Tunarejeshwa na kuelezwa jinsi babuye Imani Mwinyi Hatibu aliyefanya kazi ya kuendesha trekta katika shamba la mzungu.
(xii) Tunarejeshwa nyumbani jinsi chichiri Hamdi alivyouliwa jinsi Mtemi alivyopenda wasichana na kupatana na mmoja kiwete akiwa safarini
(10x1=10)

***HADITHI FUPI.***

***TUMBO LISILOSHIBA.***

(i) Viongozi kuweka vitego na vikwazo vya sheria ili watu wadogo wasiweze kutetea mali zao.
(ii) Kutowahusisha maskini katika maamuzi muhimu yanayoathiri maisha yao.
(iii) Kunyakua ardhi ya madongoporomoka ambapo watu maskini waliishi.
(iv) Kupanga njama za kuwapatia wanyonge visenti vichache ili waondoke madongoporomoka.
(v) Jitu la miraba mine kula chakula chote bila kubakishia wateja.
(vi) Wanamadongoporomoka kubomolewa vibanda vyao na mabuldoza.
(vii) Askari wa baraza kutimua watu waliokuwa wanabomolewa .
(viii) Jeshi la polisi kulinda askari wa baraza wakibomoa vibanda vya wanamadongoporomoka.
(ix) Askari kuwapiga virungu watu.

***SHIBE INATUMALIZA.***

(i) Mzee mambo kulipwa kwa vyeo viwili alivyovifanyia kazi.
(ii) Waajiriwa kwenda kazini na kukosa kufanya kazi.
(iii) Viongozi kuibia wananchi kwa kujipakulia mshahara
(iv) Waajiriwa wawili kufanya kazi moja – Sasa na Mbura ni mawaziri wa wizara moja.
(v) Mzee mambo kuandaa sherehe ya kuingiza watoto nasari kwa kutumia pesa za umma.
(vi) Mzee mambo kuandaa sherehe kwa kutumia rasimali za nchi- magari, vyakula.
(vii) Sasa na mbura kula vyakula vyao na vya wenzao.
(10x2=20)

7. ***FASIHI SIMULIZI.***

a) Mivigha ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii katika kipindi Fulani cha wakati. (2x1=2)

b) i) Huandamana na matendo.
ii) Huongozwa na watu mahsusi.
iii) Anayeongoza anavalia maleba.
iv) huandamana na utoaji wa mawaidha .
v) huandamana na utamaduni wa jamii husika.
(Al. 4x1=4)

c) i) Baadhi zimepitwa na wakati – tohara kwa wasichana.
ii) Baadhi hukinzana na malengo ya taifa.
iii) Baadhi hujaza hofu – utoaji kafara.
iv) Baadhi huhusisha ushirikiano.
v) baadhi huhusisha kiasi kikubwa cha pesa.
(al.2x1=2)

d) Ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee. (alama 2x1)

e) i) Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani.
ii) ni nyenzo ya kukuza ujuzi na ufasaha wa lugha.
iii) ni msingi wa kuteua viongozi.
iv) huhifadhi utamaduni wa jamii.
v) ni nyenzo ya kuburudisha jamii.
vi) hukuza uzalendo.
viii) hutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu ulio na athari kubwa.
(al.4x2=8)

8. a) Wimbo /mbolezi (2x1=2)

b) i) Hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
ii)Huimbwa kwa nia ya kufariji.
iii) Husifu aliyekufa.
iv) Hufungamana na muktadha maalum.
v) huimbwa kwa toni ya huzuni.
vi) Huibwa kwa utaratibu.

(al.4x2=8)

c) i) Takriri – wewe nenda
ii) Balagha – umeenda?
iii) Istiari – maisha ni moshi.
iv) Tashbihi – tutapaa ka malaika
v) nidaa – ooh!

4x1=4

d) i) Husawiri msimamo wa jamii kuhusu kifo.
ii) Ni kumbukumbu za aliyekufa.
iii) Hufariji waliofiwa.
iv) Ni njia ya kutakasa moyo na hisia za aliyefiwa.
v) Huendeleza utamaduni wa jamii husika.
vi) Huelimisha kuhusu mila na itikadi.
vii) Huwapa wanajamii matumaini.
viii) Huleta utangamano.
(6x1=6)

<<< M W I S HO >>>